# HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

Shule ya Sekondari Kinyanambo,

S.L.P 283,

**MAFINGA**

7/12/2020

**Kumb. Na. HM/MAF/JN/2021/01**

………………………………………………

………………………………………………

**S.L.P** ……………………………………

**MAFINGA.**

**YAH: MAAGIZO YA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukuarifu na kukupongeza kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika **Shule ya Sekondari Kinyanambo mwaka 2021.**Hongera sana!!

Shule itafunguliwa tarehe **11/1/2021** saa moja kamili asubuhi.

Tuna imani kuwa wakati wote utakaokaa Kinyanambo Sekondari utakuwa tayari kupokea , kujifunza, kutii sheria za shule, kutekeleza maagizo na taratibu za shule.

Shule ya Sekondari Kinyanambo ni ya Kutwa.

## A. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuriporti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, walimu na wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika shughuli zote ndani na nje ya shule ni muhimu.
3. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni kwa kujisomea na kumaliza kazi ulizopewa na walimu.
4. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

Scanned with CamScanner

5. Kufanya usafi wa mwili na mazingira ya shule.
6. Kujituma katika kazi zote ndani na nje ya darasa pamoja na kutunza mali zote za umma. Mfano majengo,vitabu, madawati, ndoo na vifaa vingine vyote vya shule.
7. Kuvaa Sare ya Shule wakati wote uwapo shuleni kwa kufuata taratibu za shule.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na Ushoga
3. Ulevi na madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba kwa msichana na kusababisha mimba ndani na nje ya shule kwa wavulana
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, Kuchochea, na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au wa watu wengine
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kuwa na simu ya Mkononi.
15. Kukutwa kwenye nyumba za starehe kama disco, bar, na nyumba za kulala wageni.

## B. MAHITAJI KWA WANAFUNZI WOTE WAVULANA NA WASICHANA

1. Masharti/ blauzi nyeupe yenye mikono mirefu aina ya tetroni mawili (2).
2. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi jozi mbili (2).
3. Soksi ndefu rangi nyeupe jozi mbili (2) kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
4. Suruali mbili (2) kwa wavulana na **ishonwe mshono wa heshima siyo kimodo na iwe na mfuko mmoja nyuma** siyo miwili na sketi mbili kwa wasichana zenye **malinda madogo madogo na ivuke magoti (ifunike soksi) yasiwe malinda sita. Rangi ni kijani ya mgomba pamoja na tai ndefu ya kijani ya mgomba kwa wavulana na wasichana.**
5. Kwa wasichana waislamu watashona hijabu na suruali ya heshima ambayo rangi ni kijani ya mgomba na hijabu nyeupe.
6. Nguo za michezo ni Bukta ya rangi ya blue yenye mistari myeupe na t-shirt za njano kwa wavulana na wasichana pamoja na raba za michezo rangi nyeusi zenye kamba.
7. Sweta Rangi ya kijani ya Mgomba kwani hatutaruhusu kuvaa koti au sweta ya rangi nyingine muda wote atakaokuwepo shuleni.

Scanned with CamScanner

8. Aje na truck sut za blue zenye mistari myeupe isiyokuwa na kamba miguuni na t-shirt ya njano hiyo itakuwa sare ya siku ya ijumaa ni lazima.

## C. MAHITAJI MENGINE

1. Aje na cheti cha kuzaliwa. (kivuli)
2. Daftari Kubwa Counter book kumi na tano (15) na daftari zilizoandikwa msomi kumi na moja (11).
3. Kalamu za wino sita (6), pensel tatu |(3), na mathematical set moja (1)
4. Vitabu vyakujisomea vya masomo mbalimbali ni vizuri akawa navyo ni vya kwake binafsi.
5. Mwanafunzi atatakiwa kupata chakula cha mchana shuleni, mchanganuo wa bajeti ya chakula kwa mwanafunzi umeambatishwa ambao wazazi waliukubali kwenye kikao cha wazazi na viongozi wa bodi ya shule .
6. Aje na bunda moja la Karatasi (Rim A4)

Mwanafunzi anapo riporti shuleni aje na mzazi wake au mlezi, akija bila mzazi hatapokelewa.

Mwanafunzi aje na fomu zilizoambatisha zikiwa zimejazwa, fomu hizo ni:

1. Fomu ya maelezo ya daktari (Medical certificate)
2. Fomu ya kukubali nafasi aliyopewa na kujieleza mambo binafsi (Kiambatishi A)

Tunaomba mwanafunzi akamilishe maagizo yote hapo juu ili aweze kupokelewa na kuwa na amani katika masomo yake awapo shuleni na tunaomba wazazi muwe wawazi kwa mwanafunzi mwenye matatizo ya afya ili tuweze kuwa jirani naye na kumpa ushauri kwa ukaribu zaidi.

**SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/1/2021**

**KARIBU SANA KINYANAMBO SEKONDARI**

..............................................................

**E.G. NDOKOLE**
**MKUU WA SHULE**

Scanned with CamScanner

**HALMASHAURI YA MJI MAFINGA**

**SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO**

**UCHANGIAJI WA CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI KUANZIA JANUARI 2021.**

**UCHANGIAJI CHAKULA KWA KILA MWANAFUNZI KWA KIDATO CHA KWANZA NA CHA TATU**

Wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tatu watakuja na vyakula na fedha taslimu kwa mwaka mzima kama ifuatavyo:

1. Unga wa Mahindi kilo arobaini (40kg)
2. Maharage kilo ishirini na tano ( 25kg)
3. Mchele kilo kumi na tatu (13kg)
4 Fedha taslimu arobaini na tano elfu tu. (45,000/=)

**VIFAA HIVYO UTALETA KWA AWAMU NNE;**

**1/January 2020:**

- Unga 11kg
- Maharage 7kg
- Mchele 4kg
- Fedha taslimu 15,000/=

**1/ April 2020**

- Unga 11kg
- Maharage 7kg
- Mchele 4kg
- Fedha taslimu 10,000/=

**1/ Julai/2020**

- Unga 9kg
- Maharage 6kg
- Mchele 3kg
- Fedha taslimu 10,000/=

**1/Oktoba /2020**

- Unga 9kg
- Maharage 5kg
- Mchele 2kg
- Fedha taslimu 10,000/=

**Nina waomba wazazi tuwasaidie wanafunzi wetu ili taaluma iweze KUPANDA.**

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **ESTERINA G.NDOKOLE** | **SIFA GERANA** |
| **KATIBU WA BODI YA SHULE** | **MWENYEKITI WA BODI YA SHULE** |

KATIBU WA BODI SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO

MWENYEKITI WA BODI SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO

Scanned with CamScanner

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MAFINGA TOWN COUNCIL
KINYANAMBO SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a medical officer in respect of all form one entrant)

Students full name……………………………………………………………………………………………

Age………………………………………………years, sex………………………………………………………

Blood count (Red and White)………………………………………………………………………………

Stool Examination………………………………………………………………………………………………

Syphilis and other venereal Disease Test……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

T.B Test………………………………………………………………………………………………………………

Eye Test……………………………………………………………………………………………………………

Ears……………………………………………………………………………………………………………………

Spleen………………………………………………………………………………………………………………

Abdomen……………………………………………………………………………………………………………

Urine for Plamotest……………………………………………………………………………………………

Test for pregnancy (for girls only)……………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g physical defects, Impartment e.g Infections, chronic or family disease etc)

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit pursue studies in Secondary Education

Station……………………………………………………Signature……………………………………………

Date………………………………………………………Designation…………………………………………

Scanned with CamScanner

KIAMBATISHI A

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI MAFINGA**

.........................................................................

.........................................................................

.........................................................................

.........................................................................

Tarehe.....................................................................

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO
S.L.P 283,
**MAFINGA**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KINYANAMBO.**

JINA LA MWANAFUNZI.....................................................................................
KIDATO..............................................TAREHE.....................................................

1. Mimi ...............................................................................mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu nakiri kuwa nimeyaelewa maelezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali kuchangia mchango wa chakula kwa wakati kama walivyokubaliana wazazi wenzangu kuwa suala la kupata chakula mwanafunzi shuleni ni la lazima.
3. Nakubali mwanangu ajiunge na shule hii na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kama mzazi / mlezi kwa wakati wake kama ilivyoagizwa kwenye maelekezo ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali kwa uwezo wangu wote ili kufanikisha malengo yake ya kujiunga na shule hii.
5. Naahidi kusimamia nidhamu yake wakati wote atakapokuwa kwenye shule hii.

JINA LA MZAZI / MLEZI...................................................SAHIHI.........................TAREHE..........................
ANWANI YA MZAZI / MLEZI.....................................................................................
NAMBA YA SIMU...................................................................................................

Mimi..............................................................................Niliyechaguliwa kujiunga na shule hii, naahidi kuwa mtiifu kwa sheria zote za shule na taratibu zake na kuwa na nidhamu ya kujituma kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa wanafunzi wenzangu ilikufanikisha malengo ya shule hii.Tofauti na hayo niondolewe shuleni mara moja.

JINA LA MWANAFUNZI...............................................................SAHIHI..................................TAREHE

Scanned with CamScanner